BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 26 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

135. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kuwa Serikali imeanza utekelezaji wa miradi mikubwa kama ya Ujenzi wa Barabara mbali mbali nchini.

Je, ni lini Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itaanza ukaguzi wa "Real time" ili kuhakikisha thamani halisi ya miradi hiyo inapatikana.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

153. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali kwa kuwajali wananchi wake, imeamua kuwajengea soko katika eneo la Kinyasini, Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga eneo la maegesho ya magari (parking) katika eneo hilo la soko, hasa ikizingatiwa kwa sasa kuna shida kubwa ya msongamano wa magari yanayoingia sokoni hapo.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

134. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika kudhibiti mapato ya nchi yasipotee kiholela, hivi karibuni Serikali imeanzisha mifumo ya ukusanyaji wa kodi kwa kutumia mashine za kieletroniki.

Je, ni mafanikio gani yaliyopatikana tangu mifumo hiyo ianze kutumika.

154. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Serikali Kuu imeendelea kuyadhibiti mapato yake kwa njia tofauti, ikiwa ni pamoja na mapato yaliyokuwa yanakusanywa kupitia vyanzo vya mapato vya Halmashauri na Mabaraza ya Miji. Na kwa kuwa kitendo cha Serikali Kuu kuyachukua mapato hayo kimepunguza uwezo wa Halmashauri na Mabaraza hayo kujikusanyia mapato, huku pia wanakawia kuwapa asilimia za mgao uliokubaliwa kupewa na Serikali Kuu;

(a) Je kuna sababu gani zinazopelekea Serikali Kuu kukawia kurejesha asilimia ya mgao kwa Halmashauri na Mabaraza ya Miji.

(b) Kwa kuwa hali hii imekuwepo kwa muda mrefu sasa, kwa nini Serikali Kuu isione haja ya kuvirejesha vyanzo hivyo kwa Halmashauri na Mabaraza ya Miji.

(c) Je, kuna sababu zipi zilizoipelekea Serikali Kuu kuvichukua vyanzo vya mapato vya Halmashauri na Mabaraza ya Miji.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

138. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji:

Kwa kuwa kumekuwa na taarifa nyingi zenye kutofautiana juu ya takwimu za vijana wasiokuwa na ajira Zanzibar, na kwa kuwa taarifa sahihi juu ya jambo husika zinaisaidia Serikali kupanga vyema shughuli zake.

(a) Je, ni zipi takwimu sahihi za vijana wasiokuwa na ajira nchini.

(b) Je, kiwango "rate" cha ongezeko la vijana wasiokuwa na ajira kikoje.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

156. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaishukuru Serikali kwa jitihada za kutengeneza barabara, ikiwa ni pamoja na barabara kuu na barabara zinazounganisha kijiji kimoja na kijiji chengine. Hata hivyo, barabara ya Mpapa/Pagali na Bambi Matora ni mbovu na ipo katika hali mbaya kwa muda mrefu sasa, huku ahadi zilizowahi kutolewa za kuitengeneza, hazijatekelezwa hadi leo.

(a) Je, kuna mpango gani wa kutengenezwa kwa barabara ya Mpapa/Pagali Bambi Matora.

(b) Kwa kuwa wananchi wa eneo hilo wameng'olewa mazao yao bila ya kulipwa fidia kwa muda mrefu sasa, Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi hao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

143. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Skuli ya Kilimo ya Kizimbani ndio pahala pekee ambapo hupatikana ujuzi wa kilimo na ufugaji hapa Zanzibar. Hata hivyo, kila siku zinavyokwenda, ndio miongoni mwa maeneo yanayovamiwa na wananchi kwa ujenzi wa nyumba za makaazi na shughuli zao nyenginezo.

(a) Je, Wizara yako inatoa kauli gani juu ya uvamizi unaofanywa na baadhi ya wananchi walio karibu na maeneo ya skuli hiyo.

(b) Ni hatua gani zilizochukuliwa juu ya wananchi hao.

<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>

28. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika moja ya ziara zake za kikazi katika jimbo la Mfenesini, Mhe. Waziri aliyepita wa Wizara yako, aliwaahidi wananchi wa Shehia ya Bumbwisudi kwamba, Serikali baada kusikiliza kwa makini kilio cha wananchi wa Bumbwisudi, imeamua kuwapatia wananchi hao kisima kimoja kati ya visima saba vinavyopeleka maji mjini, ili kuweza kuwahudumia wananchi wa kijiji hicho waondokane na shida ya ukosefu wa maji.

(a) Kwa kuwa ahadi ni deni na hasa hii iliyotolewa zaidi ya mwaka mmoja hivi sasa, Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

(b) Kwa kuwa wananchi hao kwa sasa wanategemea maji kutoka kisima cha Ndagaa, na kwa kuwa kisima hicho cha Ndagaa nacho hakina uwezo wa kutoa huduma kwa majimbo ya Uzini na Mfenesini. Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu ili kumaliza kero hiyo.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

45. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Chukwani ni skuli inayosomesha wanafunzi kuanzia msingi hadi sekondari ya juu (Advanced level) kwa masikitiko skuli hii ipo katika hali mbaya sana na hatarishi kwa walimu na wanafunzi ukizingatia baadhi ya viongozi wa kitaifa washajionea hali halisi na haikuwaridhisha.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuirudisha skuli ya Chukwani iwe inaendana na hadhi ya skuli za kisasa.

124. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwakuwa kumekuwa na kilio cha wanafunzi wenye ulemavu wa uziwi katika kujifunza na hata katika kufanya mitihani yao.

Je, Serikali ina mpango gani kwa wanafunzi wa aina hiyo kwa ajili ya kuwawekea mazingira wezeshi yatakayotambua na kurahisisha mitihani yao kwa mujibu wa ulemavu wao.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2021/2022.



Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
26 Septemba, 2022. KATIBU WA BARAZA.